

## **Mtagusano wa Uolezi na Uhusika katika Uwasilishaji wa Ujumbe katika Riwaya ya Kiswahili**

*Dinah Sungu Osango*<sup>1</sup>  
Chuo Kikuu cha Nairobi

*Mwenda Mbatiah*<sup>2</sup>  
Chuo Kikuu cha Nairobi  
na

*Timammy Rayya*<sup>3</sup>  
Chuo Kikuu cha Nairobi

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.7>

### **Ikisiri**

Makala haya yanachanganua mtagusano wa uolezi na uhusika katika riwaya teule za Kiswahili ili kuonesha jinsi aina mbalimbali za uolezi zinavyoathiri ujenzi wa wahusika na kushawishi uibukaji wa ujumbe katika riwaya za Kiswahili. Uchanganuzi wa uolezi ni muhimu katika kutuonesha jinsi waandishi wanavyowatumia wahusika ili kuangazia masuala ya jadi au masuala ibuka ya kisasa katika jamii kwa kutumia mitazamo mbalimbali; na kwa njia hiyo, kufanya uolezi na uhusika kuwa mkakati wa kuwasilisha ujumbe mahususi kwa wasomaji. Uchunguzi wa suala la uolezi katika riwaya za Kiswahili unatokana na tafiti zilizopo kudai kuwa, uolezi ni suala ambalo halijatiliwa maanani katika tafiti za kifasahi zinazoangazia usimulizi wa riwaya ya Kiswahili. Riwaya ambazo zimetumiwa katika uchanganuzi wa makala haya ni: *Haini* (S.A. Shafi, 2002), *Makuadi wa Soko Huria* (C.S.L. Chachage, 2005), *Ndoto ya Almasi* (K. Walibora, 2006), *Nyuso za Mwanamke* (S.A. Mohamed, 2010), *Harufu ya Mapera* (K.W. Wamitila, 2012) na *Hujafa Hujumbika* (F.M. Kagwa, 2018). Kwa kuwa riwaya hizi zina mawanda mapana, tumedondoa tu baadhi ya mifano ambayo inadhihirisha uolezi na uhusika ili kupata data ambazo zimetupa picha kamili kuhusu riwaya ya Kiswahili. Madhumuni ya uchanganuzi huu ni kutambulisha aina mbalimbali za uolezi na uhusika na uamilifu wake katika uwasilishaji wa simulizi. Uchunguzi huu umeongozwa na Nadharia ya Naratolojia ambayo inatambua uolezi na uhusika kama vipengele muhimu katika uwasilishaji wa simulizi.

### **1.0 Utangulizi**

Uolezi ni mtazamo wa kiutunzi na kisha wa kiuchanganuzi ambao hutumiwa kuangazia mkabala wa uwasilishaji wa hadithi katika riwaya au simulizi yoyote ile. Uolezi unajishughulisha kuangazia na kutathmini swali: 'ni nani anayeona

<sup>1</sup> Barua pepe: [osangodinah72@gmail.com](mailto:osangodinah72@gmail.com)

<sup>2</sup> Barua pepe: [ammbatiah08@gmail.com](mailto:ammbatiah08@gmail.com)

<sup>3</sup> Barua pepe: [rayya@uonbi.ac.ke](mailto:rayya@uonbi.ac.ke)

kinachosimuliwa katika riwaya au simulizi?' Uolezi ni kijenzi kimojawapo cha simulizi ambacho kinaonesha mshikamano kati ya uhusika na uwasilishaji wa simulizi. Istilahi hii ilibuniwa na wananadharia ya Naratolojia kurejelea kile ambacho katika uhakiki wa kijadi kinajulikana kama mtazamo-kitazamio. Kwa mujibu wa Abrams (1993), uolezi ni dhana inayorejelea jinsi hadithi inavyowasilishwa, yaani ni njia ambazo mwandishi anazitumia kuwasilisha kwa msomaji wahusika, dayalojia, matendo, mandhari na matukio yanayounda simulizi katika kazi ya bunilizi. Hawthorn (2010) anasema kwamba istilahi ya 'mtazamo haipambanui ni nani msemaji, nani anayeona na ni nini anachoonika katika simulizi. Hii ndiyo sababu hapo awali Genette (1972) aliibuni istilahi hii ya uolezi ili kuwezesha masuala yaliyobainishwa hapa kwa ubayana. Kupitia uolezi, tunaweza kutambua iwapo ni mwandishi aliyeyashuhudia matukio au anamtumia mmojawapo wa wahusika ili kuwasilisha ujumbe wake.

Uolezi ni kipengele muhimu ambacho hutumiwa na wasimulizi ili kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji kama walivyofafanua wanataaluma wengi katika Nadharia ya Naratolojia. Pia, uolezi unatuwezesha kuainisha wasimulizi kama vile msimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi wa nafsi ya pili na msimulizi wa nafsi ya tatu (Genette, 1972). Uainishaji huu ni muhimu kwa sababu kila mwandishi huchagua aina ya msimulizi wa kuwasilisha simulizi ya kazi yake kulingana na malengo yake. Hii ina maana kwamba uteuzi wa msimulizi ni kigezo cha msingi kinachomdokezea msomaji mambo mengi katika simulizi, yanayojumuisha ujumbe wa kazi inayohusika. Muhimu zaidi ni kwamba uolezi unatuwezesha kuchanganua tajiriba, hisia na mitazamo ya wahusika mbalimbali wa kazi inayohusika. Namna wanavyoona, wanavyohisi na wanavyowaza wahusika ni kiashiria muhimu cha kile kinachohusika na kinachowasilishwa kwa msomaji.

Kwa upande mwingine, uhusika ni kipengele cha simulizi ambacho ni muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe. Uhusika unaweza kufafanuliwa kama mbinu ya kuwasilisha wasifu, hulka na tajiriba mseto za wahusika katika simulizi kwa kadiri ya uchangamano wa mitagusano yao. Dhana hii inachukuliwa kama mchakato wa kuunda sifa za wahusika (Chatman, 1978; Wamitila, 2002) ambapo watunzi wa kazi za fasihi huwateua wahusika fulani na kuwapa sifa mbalimbali kulingana na malengo yao ya utunzi. Wanazuoni kama vile Senkoro (1987) na Wamitila (2002), wanaeleza kuwa wahusika ni viumbe ambao wanapatikana katika kazi ya fasihi; ni viumbe mahususi na amilifu ambao wanaweza kuwa watu, wanyama, mimea, majini au vitu visivyo na uhai kama vile mawe lakini ambavyo vimeukiliwa kutekeleza majukumu anuwai katika kazi husika. Wahusika huwa nguzo kuu katika kuasisi na kuibua mawasiliano katika kazi ya kisanaa kwa kuwa wao ndio hubebeshwa jukumu la kutenda, na kwa hivyo, kusababisha matukio na katika harakati hiyo sifa zao huweza kubainika. Kupitia mitagusano ya wahusika anuwai, ujumbe mbalimbali hudhihirika katika simulizi, si kwa sadfa, lakini kwa njia mahususi kama alivyodhamiria mtunzi wa kazi. Ndiyo kusema kuwa msomaji

anastahili kufahamu maana ya viambajengo vya lugha iliyotumiwa na wahusika au msimulizi katika tungo na kuihusisha maana hiyo na miktadha husika ili kufahamu alichokusudia kuwasilisha msimulizi. Hivyo basi, kwa kuzingatia uelewa huo, makala haya yanachanganua mtagusano wa uolezi na uhusika kadiri unavyojitokeza katika riwaya teule za Kiswahili ili kuonesha jinsi aina mbalimbali za uolezi zinavyoathiri ujenzi wa wahusika na zinavyoshawishi uibukaji wa ujumbe katika kazi husika.

## **2.0 Msingi wa Nadharia**

Mjadala unaoibuliwa na kuendelezwa katika makala haya umekitwa na kuegemezwa katika Nadharia ya Naratolojia. Uchunguzi wetu unaongozwa na mawazo ya mwananaratolojia Gerard Genette (1972) ambaye ndiye mwasisi wa istilahi ya uolezi. Genette na wananaratolojia wengine kama vile Vladimir Propp (1968) na Seymour Chatman (1978), walipendekeza kuchambua simulizi kwa kurejelea kilongo. Hivyo basi, wananadharia hao walitunga sheria ambazo zilifaa kudhibiti riwaya kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Kwa mfano, Genette (1972) alichangia katika ukuzaji wa nadharia hii pale ambapo katika uhakiki wake anaonesha mambo matatu muhimu ya kuzingatia katika simulizi ambayo ni matini, hadithi na usimulizi. Pia, anapendekeza kutofautishwa kwa yule anayesimulia na yule anayeona matukio. Kwa hivyo, anapendekeza neno uolezi ili kudhihirisha anayeona kitendo, tajiriba au tukio fulani. Ili kufafanua zaidi kuhusu uolezi, anaeleza aina tatu za uolezi, yaani uolezi ndani, uolezi nje na uolezi nunge. Aidha, Genette anasisitiza umuhimu wa kumtofautisha mtu anayesimulia hadithi na yule anayeona matukio katika hadithi na huu ndio msingi wa dhana ya uolezi.

Uundaji wa istilahi ya uolezi uliwachochea wananaratolojia wengine kufanya utafiti zaidi. Licha ya kuwa Genette ndiye aliyependekeza matumizi ya istilahi ya uolezi ili kutatua utata uliokuwapo hapo awali kuhusu tofauti kati ya anayesimulia hadithi na yule anayeona matukio, maelezo yake yalikuwa ya kijumla. Kutokana na hali hii ndipo kukawa na tafsiri anuwai za istilahi hii, ambapo wanazuoni mbalimbali wamekuwa wakiifafanua kwa njia tofautitofauti huku wakitunga sheria za kuidhibiti. Hata hivyo, mawazo ya Genette ndiyo yaliyotuchochea kuchanganua na kutathmini dhana ya uolezi na kutambua umuhimu wake katika riwaya ya Kiswahili.

Licha ya kuwa nadharia hii ina mihimili mingi, ukuzaji na uendelezaji wa mjadala katika makala haya umekitwa katika mihimili michache inayoendana na malengo ya makala haya. Kwanza, tumetumia mhimili wa uolezi ambao unajibainisha kama kipengele muhimu katika simulizi. Huu ni mhimili muhimu katika kutambua aina za uolezi zinazoweza kujitokeza katika riwaya kama tunavyokusudia kuonesha katika riwaya teule zinazotumiwa katika makala haya.

Mhimili mwingine ambao umetumika katika mjadala wa makala haya ni wa usimulizi unaowezesha kubainika kwa masuala ya mawasiliano ya binadamu. Usimulizi ni kipengele muhimu kwa kuwa ndani yake mnabainika aina mbalimbali za usimulizi zinazojenga uhusiano kati ya kile kinachosimuliwa na matumizi ya lugha. Kuwapo kwa aina mbalimbali za usimulizi, kunawezesha utambuizi wa aina tofauti za uolezi.

Aidha, tumetumia mhimili wa uhusika ambao ni muhimu katika ubainishaji na utabakishaji wa wahusika na sifa za wahusika kutokana na maelezo ya msimulizi kuhusu tabia zao au kupitia matendo, kauli za wahusika wengine, majina ya kimajazi au kupitia mwonekano wao wa nje.

### 3.0 Aina za Uolezi

Wanazuoni kama vile O’Neil (1994), Rimmon-Kenan (2002) na Bal (2009) wanakubaliana kuwa kuna aina mbili za uolezi ambazo ni uolezi ndani na uolezi nje. Njia hizi mbili hutambulishwa kutokana na mahali aliko muolaji wakati wa usimulizi wa hadithi. Iwapo muolaji yuko karibu au ndani ya hadithi, basi, tunakuwa na uolezi ndani na iwapo muolaji yuko mbali au nje ya hadithi tunapata uolezi nje.

### 3.1 Uolezi Ndani

Uolezi ndani hutambuliwa kupitia usimulizi ndani kwa uelewa kwamba msimulizi ndani anaweza kuwa mhusika aliye ndani ya hadithi na ambaye anashiriki katika matukio, au mtazamaji tu ambaye anaripoti yale yanayotukia wakati anayatazama. Kwa hivyo, huwa anayasimulia matukio ya hadithi huku akiola. O’Neil (1994) anamwita muolaji wa aina hii mhusika-muolaji. Aina hii ya uolezi inadhihirika katika riwaya zilizoteuliwa. Kwa mfano, katika *Makuadi wa Soko Huria* uolezi ndani unadhihirika wakati msimulizi anaposema:

Tulifika Kibiti mnamo saa mbili za usiku wakati wa giza ndio kwanza linaingia. Mimi na Bwana Ibwe tulikuwa macho, wengine wote walikuwa wamelala usingizi baada ya kuondoka kijiji cha Kimanzichana. Haya yote yalikuwa ni matokeo ya unywaji pombe uliofanyika wakati keria ya gari inatengenezwa... (uk. 135).

Katika dondoo hili viwakilishi “mimi” na “tu” vinaashiria msimulizi ndani ambaye anasimulia hadithi akiwa na wahusika wenzake wengine walioshiriki naye katika matukio ya hadithi. Katika riwaya hii, matukio mengi yanasimuliwa kupitia wahusika ambao wako ndani ya hadithi. Kwa hivyo, anayeona matukio ni Fidelis Mvumi Msakapanofu na wahusika wengine wa karibu kama vile Binti Wenga. Aidha, katika riwaya hii, msimulizi anajitambulisha moja kwa moja kwa kuonesha kuwa yeye ndiye anayeyasimulia matukio ya hadithi. Usimulizi wa aina hii hujenga uhusiano wa karibu kati ya msimulizi na msomaji. Hali hii inamfanya msomaji

kutaka kujinasibisha na mhusika anayepatikana katika simulizi husika. Kwa mfano, msimulizi anajitambulisha moja kwa moja katika mifano ifuatayo:

Mimi mwenyewe ni mhusika pia katika mambo yaliyotokea lakini kwanza nimalizie kujitambulisha. Ninajulikana kwa jina kamili kama Fidelis Mvumi Msakapanofu. Nimeishi sehemu mbalimbali za nchi... Mimi mwenyewe nimekuwa nafanya kazi kama mwandishi wa habari, tangu mwaka 1975... Lakini ninayokusudia kuandika hapa si habari bali ni mambo na matukio... (uk. 10).

Kinachothibitika katika muktadha huu ni kwamba msimulizi anayasimulia mambo mengi aliyokumbana nayo katika maisha yake alipokuwa akiishi katika sehemu mbalimbali za nchi ya Tanzania. Kwa kuwa msimulizi amejitambulisha moja kwa moja, msomaji anavutwa karibu na hisia zake, na angependa kufahamu ni yapi yaliyomwathiri katika maisha yake. Katika hali hiyo, ujumbe uliokusudiwa na mwandishi unamfikia msomaji. Kupitia kwa mhusika-muolaji, msomaji anaweza kujua mtazamo, tabia na sifa zake na zile za wahusika wengine anaokabiliana nao. Fidelis na wenzake wanaathirika kutokana na mapambano ya kisiasa yanayosimuliwa katika riwaya hii.

Muolaji ndani hujikita katika yale anayoyaona na kufahamu, kwa hivyo, huwa ana ufahamu mdogo kuhusu tajiriba za wahusika wengine ambao hajahusiana nao moja kwa moja, pia hana uwezo wa kuyasoma mawazo ya wahusika wengine (Rimmon-Kenan, 2002). Genette (1980) anatumia mtindo ufuatao ili kuelezea hali hii: msimulizi = muolaji; yaani, msimulizi huwa katika kiwango sawa na yule anayeyaona matukio. Iwapo atasimulia yale yaliyotokea kitambo, basi yeye hujua mengi kuliko msomaji kwa kuwa huwa anasimulia mambo ambayo yeye ameshayashuhudia maishani mwake. Kinyume na hayo, mhusika-muolaji ambaye anasimulia matukio yanayoendelea kutokea huwa hana ufahamu wa mambo mengi hasa yale ambayo yatatokea baadaye. Katika hali hii, mara nyingi mhusika-muolaji humwacha msomaji katika hali ya taharuki. Mfano ufuatao kutoka katika riwaya ya *Hujafa Hujaumbika* unadhihirisha hali hiyo: “*My God, why me? Why at this time? Ooh no my Lord! Kwa nini Mungu waruhusu hili litendeke kwangu? Kumbuka hata sijalipa mko...*” (uk. 39).

Katika nukuu hapo juu, msomaji anamwona Bi Timazi kupitia Mwanga ambaye ni mwanawe. Anaposikia tangazo kwenye runinga kuhusu kufutwa kwake kazi, anakumbwa na huzuni nyingi na majuto. Katika nukuu hapo juu, alikuwa ameanza kusema jambo kuhusu mkopo lakini hakukamilisha. Katika muktadha huu, msomaji anaachwa katika hali ya taharuki kwani hafahamu hasa ni nini alichokuwa akirejelea. Kwa kuwa Mwanga hana ufahamu wowote kuhusu mkopo uliokuwa ukirejelewa, hamfafanulii msomaji kuhusu mkopo huo. Hata hivyo, ujumbe kuhusu

mkopo unafafanuliwa baadaye katika hadithi kupitia Bi Timazi anapowaeleza wanawe sababu ya yeye kufutwa kazi.

Katika *Nyuso za Mwanamke*, mwandishi anatumia uolezi ndani kwa vile wahusika wakuu ndio wanasimulia matukio yanayowahusu. Faisal na Nana wanapewa jukumu la kusimulia matukio yanayowahusu katika shughuli mbalimbali za kimaisha. Katika uolezi ndani, msomaji huvutwa katika ulimwengu wa msimulizi. Akiwa huko huyahisi yale ambayo msimulizi anayashuhudia na huathiriwa nayo. Kwa mfano, kupitia uolezi ndani, tunapata hisia za ndani za Nana kuhusu hali yake ya maisha akiwa nyumbani kwa baba yake anaposema:

Ndivyo nilivyopanga mimi mwenyewe, ingawa sivyo nilivyotarajia... Yaani sikutazamia kwamba angekasirika kiasi kile... Sikudhani kwamba angevuka mipaka. Lakini hivyo ndivyo nilivyotaka iwe hatimaye. Nilikuwa natafuta sababu na sasa nimepata sababu. Nimechoka kuvumilia (uk. 48).

Nikalia kwa kekefu huku nikimiminika machozi yaliyotoka ndani ya tungi langu la hisia. Amenipiga baba hatimaye. Amenipiga mimi jituzima. Mimi mwenye uhuru wa kuchagua namna maisha yangu ninavyotaka yawe- mabaya au mazuri, amenipiga (uk. 48).

Katika dondoo hili, mwandishi analenga kuonesha hisia za Nana zilizomfanya aamue kutoroka nyumbani kwao. Hisia za uchungu, majuto na chuki zinadhihirika katika dondoo hili. Nana anasimulia matukio yake mwenyewe akiwa nyumbani kwa baba yake. Hii ni baada ya baba yake kumwandalia sherehe kubwa ya kubalehe kwake na kufaulu katika masomo ya kidato cha sita. Hii ilikuwa mojawapo ya sherehe nyingi zilizokuwa zikiandaliwa mara kwa mara na baba yake, lakini ambazo Nana hakuzichangamkia hata kidogo. Katika sherehe hiyo ndipo Nana alipoamua kumuasi baba yake kwa kumwalika mpiga-gitaa ambaye alitoka katika tabaka la chini kinyume na masharti ya baba yake aliyewadharau watu wa tabaka hilo. Mwaliko huu ulimfanya baba yake kumzaba kofi ambalo lilizua mgogoro mkubwa kati yake na binti yake. Kwa kuwa hapo awali Nana alikuwa akiipinga mitazamo ya baba yake, alichukua fursa hii kufanya uamuzi wa kutoroka nyumbani kwao.

Uolezi ndani unaweza pia kujitokeza katika simulizi za nafsi ya tatu iwapo umbali wa wakati na umbali wa kisaikolojia kati ya msimulizi na mhusika ni mfupi. Bal (1985), Jahn (1996) na Rimmon-Kenan (2002) wanaita aina hii uolezi mseto kwa maana kuwa unabadilika kutoka aina moja hadi nyingine kama inavyodhihirika katika dondoo hili kutoka katika riwaya ya *Harufu ya Mapera*:

Cassandra alishusha pumzi, akasonya na kutikisatikisa kichwa chake kama kawaida yake katika hali hii. Akashangaa ni kwa nini mumewe alishindwa kumwelewa. Hivi ndivyo walivyo wanaume

wote? Unaishi na mtu bila kujua kama anakupenda kweli au anaishi nawe iwe yawe tu! (uk. 258).

Muktadha huu unadhihirisha jinsi ambavyo msimulizi amebadilisha uolezi wa kutoka wa nje hadi wa ndani. Dondoo linapoanza, muolaji anadhihirika kuwa nje ya hadithi, lakini kadiri simulizi inavyoendelea, sauti ya mhusika inasikika. Maneno yaliyopigiwa mstari yanadhihirisha kuwa anayeola si msimulizi ila Cassandra ambaye ni mmoja wa wahusika katika hadithi. Licha ya kuwa uolezi unaojitokeza ni wa nje, ni wazi kwamba yale maneno yaliyopigiwa mstari ni ya Cassandra. Msimulizi anayatumia maneno hayo moja kwa moja kama yalivyosemwa na mhusika kwa kuwa anataka kusisitiza hisia za Cassandra kuhusu mtazamo wake kwa wanaume. Itikadi yake kuhusu wanaume inadhihirika. Anaamini kuwa wanaume wote hawawezi kuaminiwa.

Katika *Haini*, msimulizi-muolaji ametumia uolezi ndani kudhihirisha mawazo ya baadhi ya wafungwa waliokuwa katika gereza la Kumbakumba. Kwa mfano, anasema:

Shadidi alipokuwa akiendelea na mapishi yake, macho ya Masanja yakiangaza juu ya dari ya chumba, hajui anachokitazama, ameshangaa. “Nini kilichonileta hapa? Nini?” Anajiuliza. Lakini kilichompeleka Masanja pale ni njaa. Njaa ilimshika, nchini hakuna chakula, akaona... (uk. 24).

Maneno yaliyopigiwa mstari ni ya Masanja anapojiuliza maswali kadhaa kuhusu kushikwa kwake. Anajutia uamuzi wake wa kwenda sokoni siku hiyo ili kununua unga wa magendo. Alipokuwa huko ndipo alipokamatwa na polisi waliokuwa kwenye msako wa kuwatafuta wahalifu wa kosa la uhaini. Baada ya maswali ya Masanja, msimulizi anaendelea na usimulizi katika nafsi ya tatu na kumjulisha msomaji sababu iliyokuwa imemfanya kuwa kizuizini.

Uolezi ndani pia hudhihirika kupitia mawazo akilini, mazungumzo, mahojiano na hata uzungumzi nafsia. Usemi halisi hutumiwa na wasimulizi wengi ili kudhihirisha mazungumzo na mahojiano. Wanazuoni kama vile Chafe (1994), Tannen (1989) na Clark na Gerrig (1990) wanakubaliana kuwa matumizi ya usemi halisi hudhihirisha sifa za sauti simulizi na matumizi ya ishara ambayo husaidia katika kutambua hisia za msimulizi. Katika hali kama hizo inawezekana kutowatofautisha wasimulizi na waolaji. Kwa mfano, katika *Haini*, msimulizi mara kadhaa ameamua kusimulia matukio kupitia mazungumzo licha ya kuwa mtindo wa uolezi nje umeitawala riwaya hii. Mazungumzo yanadhihirika miongoni mwa wafungwa waliokuwa wametuhumiwa kwa kosa la uhaini kama ilivyo katika mazungumzo yafuatayo:

“Tutashtakiwa?” aliuliza Ambar. Sasa amekaa sawasawa, haangalii tena juu ya dari ya chumba.

“Ndiyo.” Alijibu Hamza.  
 “Tutashtakiwa kwa kosa gani?”  
 “Kwani humu ndani tumewekwa kwa kosa gani?”  
 “Hawa watu unafikiria wana muda wa kumpeleka mtu mahakamani? Sidhani. Hawa watakuja kututoa siku moja usiku, watupige risasi sote, hakuna kesi hakuna baba yake kesi,” alisema Sururu (kur. 106-107).

Kupitia mazungumzo kati ya wafungwa hao, msomaji anaweza kupata hisia zao. Tangu walipofungwa katika gereza la Ba Mkwe, muda mrefu umepita sasa wakiwa humo bila kufahamu hasa kosa lao wala kujua iwapo watashtakiwa au la. Hofu yao ni kwamba huenda wakafyatuliwa risasi na kuuawa kiholela. Kupitia uolezi ndani, dhuluma na unyanyasaji wa wafungwa unadhihirika kwani wameyapitia mateso mengi kama vile kupigwa kinyama, kuishi katika mazingira duni, kukosa chakula na kunyimwa haki ya kufikishwa mahakamani ili kujitetea. Jambo hili linadhihirisha jinsi viongozi waliochukua hatamu za uongozi baada ya mkoloni kuondoka wanavyoendeleza mbinu za kidhalimu za kikoloni ili kuuendeleza utawala wao wa kiimla.

Kama tulivyosema hapo juu, uolezi ndani pia unaweza kudhihirika kupitia uzungumzi nafsia. Kwa kutumia uzungumzi nafsia, mwandishi anawaelekeza wasomaji kwenye fikra za wahusika ambao mara nyingi hawakusudii kusikiwa na hadhira au wahusika wengine (Hirsh, 2003). Uzungumzi wa aina hii unaweza kuwa: (1) unailenga hadhira au wahusika wanaozungumziwa, (2) usemi usioilenga hadhira au mhusika yeyote, na (3) usemi unaojitokeza katika mawazo ya mhusika fulani. Katika aina ya tatu, msomaji anapata fursa ya kuyaona maisha au tajriba za wahusika kwa kutazama fikra za wahusika hao. Katika riwaya teule za Kiswahili, mbinu hii imetumiwa na waandishi ili kufanikisha uhusika na wakati huo ujumbe uliokusudiwa ukiwasilishwa. Uzungumzi nafsia unajitokeza katika *Harufu ya Mapera* wakati Sofia anamsikitikia Maria kwa kuwa kuna mambo mengi yaliyotendeka kitambo, Maria akiwa mdogo na ambayo yanamwathiri hadi sasa. Anasikika akisema, “Maskini Maria sijui kama anayajua yaliyofichwa na ulimwengu huu!” (uk. 404).

Kauli ya Sofia inatokea bila matarajio kwani alikuwa katika mawazo na bila kukusudia anajisemea maneno hayo. Hili linadhihirika kwa kuwa baada ya kauli hiyo kumtoka kinywani, anaangalia mbele na nyuma ili kuona kama kulikuwa na mtu karibu yake aliyesikia maneno yake. Anachukua tahadhari hii kwa sababu yale aliyoyafahamu kumhusu Maria yalikuwa siri na hatari kwa kuwa hakuna aliyetaka kuyasema kutokana na hofu ya kuingia matatani. Maria alikuwa amedanganywa kuhusu kifo cha mama yake na mahali alipokuwa ameonyeshwa kama kaburi la mama yake hapakuwa na chochote ila mchanga uliokuwa umeinuliwa tu.



Mkondourazini ni mbinu muhimu katika ukuzaji wa wahusika katika kazi za kifasihi (Wamitila, 2008). Mbinu hii hulenga kuonesha mawazo yanayompitia mhusika katika mkondo wake wa ung'amuzi. Mbinu hii hufanikisha udhihirishaji wa uolezi ndani hasa wakati ambapo mhusika anawaza kuhusu mambo yanayomhusu. Mawazo ya akilini yanapotumiwa kuwasilisha ujumbe, sauti ya usimulizi huwa imepunguzwa kiasi cha kusikika tu na msimulizi (Rimmon-Kenan, 2002). Sauti ya usimulizi hufichika kiasi cha kuchukuliwa kuwa haipo katika matini simulizi. Ili kutambua aina ya uolezi katika hali kama hii, tunajiuliza ni nani anayeona. Utambulishaji huu unatuwezesha kujua iwapo ni uolezi ndani ambao umetumiwa ili kuwasilisha ujumbe. Matini ya msimulizi itaiga kibubu mtazamo wa muolaji na udhaifu wa kimawazo, ubora wa sauti ya msimulizi utasalia kutoonekana (Jahn, 2005). Mfano ufuatao kutoka katika *Ndoto ya Almasi* unadhihirisha hisia za msemaji kupitia mawazo akilini kama ifuatavyo:

Masikini nimelenga, nimelenga mazuri mengi yenye kutajika,  
nimelenga nikakosa kufuma. Kulenga si kufuma. Huenda ni  
hekima sasa kukubali nijaliwalo kuliko nitakayo...  
Laiti dunia ingekumbuka kuwa siku moja palikuwa na mtu  
aliyezaliwa Cherangani akalenga, akalenga sana, lakini  
hakufuma. Lakini siamini dunia hii ... (uk. 166).

Kupitia mawazo haya, Almasi anajutia maisha yake hasa baada ya kujaribu kila awezalo ili kufanikiwa maishani lakini kila mara alipojaribu juhudi zake hazikufua dafu. Mawazo haya yanatokea baada ya yeye kutambua kuwa Masasi Junior hakuwa mwanawe ila alikuwa mtoto wa baba yake mzazi (Mzee Masasi). Hii ni baada ya mkewe Chebosio kukiri kuwa alikuwa amemsingizia Almasi kuwa baba yake Junior. Aidha, Chebosio anamwambia Almasi sababu ya kutosema ukweli kuhusu baba mzazi wa mwanawe. Hii ni kwa kuwa, kwanza, Mzee Masasi alikuwa kama baba yake kwa kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mama yake baada ya baba yake mzazi kuaga dunia. Pili, huyo baba mkwe alikuwa amemlazimisha kujihusisha kimapenzi naye na ni kutokana na uhusiano huu ndipo alipopata ujauzito. Aidha, Chebosio alisema kuwa alitaka kuepuka aibu na masimango kutoka kwa jamii. Suala la itikadi linajitokeza hapa kwa kuwa jamii husika hairuhusu uhusiano wa kimapenzi kati ya mtu na mkaza-mwana wake. Baada ya Almasi kupata habari hizi, anajisaili ndani kwa ndani huku akitaka kujua hasa ni wapi alipokosea. Uolezi ndani unatuwezesha kufahamu kuwa kufikia sasa, Almasi ametamauka, hasa baada ya kujaribu kila awezalo ili kuyaendeleza maisha yake kwa njia halali.

Mwandishi wa *Haini* ametumia sauti ili kuwasilisha mambo yaliyokuwa yakimsumbua Pwacha akilini kama ifuatavyo:

... Pwacha alisikia sauti zikimpigia kelele na kumlaani,  
“Mzandiki! Mzandiki! Mzandiki!”

Na yeye akizijibu kimya kimya, “Mnafiki gani, sina unafiki wowote, kwa kunusuru maisha yangu hakuna unafiki wala uzandiki,”

... akiwa macho na usingizini, zinamlaani na kumpigia kelele, “Mnafiki ! Mzandiki !” (kur. 203- 204).

Pwacha anaonekana ana hisia za majuto baada ya kumsaliti Haramia kwa uongozi wa Ba Mkwe. Haramia alikuwa amewachochea wafungwa wenzake ili wakatae ushauri wa viongozi wa jela la Ba Mkwe wa kuwashawishi baadhi ya wafungwa kutoa ushahidi wa uongo uliolenga kuwatia wenzao matatani. Pwacha, Haramia na wafungwa kadhaa wakiwa chumbani walimokuwa wamefungiwa, walikuwa wamejadiliana kuhusu suala hilo, ndipo Haramia akawaonya wenzake dhidi ya hatari iliyowakabili iwapo wangekubali kutoa ushahidi wa uongo. Kwa kuwa Pwacha alikuwa kibaraka wa viongozi hao, aliwaambia kisiri mpango wa Haramia wa kukana kesi hiyo na jinsi alivyokuwa amewashawishi wenzake kuyakana mashtaka waliyopangiwa. Ujumbe huu ulipowafikia wakuu wa jela hiyo, walikasirika sana kwa kuwa waliona kwamba wafungwa hao walikosa hisani baada ya kutengewa chumba maalumu walimopata huduma bora kuliko wafungwa wengine. Baada ya kuusikia mpango wa Haramia, viongozi hao wakiongozwa na Kanali Bunju waliamua kumpeleka Haramia Mashakani Hotel alikofungiwa pamoja na chatu katika chumba kimoja. Akiwa humo, alipigana na chatu hadi akafanikiwa kumuua kwa kumuuma shingoni. Baadaye alirudishwa katika chumba chao kule gerezani alipokuwa sasa akilia kwa uchungu. Kila mara Pwacha alipomtazama, alipatwa na majuto kwa kitendo chake cha kumsaliti.

Waandishi wengine wametumia mbinu ya barua ili kuwasilisha ujumbe wa muolaji ndani. Katika barua za aina hii, hisia za muolaji huwa zimezingatiwa. Kwa mfano, katika *Ndoto ya Almasi* msimulizi anatumia barua ili kuonesha maneno kamili ya Magdalena Makabila kwa mwanawe ambaye aliaga dunia. Barua hii imebeba ujumbe muhimu wa siri iliyokuwa imefichika kwa miaka mingi kati ya Magdalena na mumewe bwana Makabila. Mfano ufuatao ni sehemu tu ya barua hiyo:

Usitusahau sisi wazazi wako. Umkumbushe Muumba juu ya taabu zetu na hasa hali yangu na huyu Makabila uliyemdhanika kuwa babako mzazi. Nafikiria jina lake haliko huko mbinguni kutokana na madhambi yake mengi. Hata mimi nilikuwa mkosaji. Niliposhika mimba yako nilitaka kuitoa kwa kuwa mwenye kuitunga hakuwa mume wangu Makabila... (uk. 127).

Kupitia barua hii, Magdalena anasimulia dukuduku lake la moyoni na siri zake ambazo ni yeye pekee anazifahamu. Barua inamjulisha msomaji kuwa bintiye Magdalena alikuwa ameaga dunia miaka kadhaa iliyopita. Kifo chake kilitokana na jaribio lake la kuavya mimba ambayo alikuwa ameipata kabla ya kuolewa. Kupitia barua hii, msomaji anapata mtazamo wa Magdalena kuhusu uavyaji mimba kwani hata yeye alikuwa amekumbwa na tatizo la kutungwa mimba isiyokuwa ya mume

wake na akafanikiwa kuificha kwa miaka mingi. Inatokea kisdafa kuwa yule mwana aliyekuwa amefichwa asili ndiye huyu aliyekuwa ameaga dunia. Barua hii inadhihirisha uovu ambao unaendelea katika baadhi ya ndoa ambapo kuna kutoaminiana kati ya mke na mume. Uovu huu unaendelea kwa muda mrefu bila ya wahusika wengine kuutambua. Magdelina anadhihirisha usiri wake kwa kuficha ukweli wa tabia yake kwa muda mrefu. Kwa kuwa aliamua kuiandika barua ya aina hii, kisaikolojia alikuwa ameyajutia matendo yake na alitamani sana kupata msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

### 3.2 Uolezi Nje

Hadithi ambayo husimuliwa kupitia uolezi nje huwa na msimulizi aliye nje ya hadithi (Rimmon-Kenan, 2002). Msimulizi-muolaji huwa na sifa za kiungu za kuweza kupenya ndani ya akili za wahusika na kuelezea mawazo na hata mitazamo yao. Msimulizi-muolaji wa aina hii huwasilisha hadithi kupitia usimulizi maizi. Usimulizi wa aina hii humwezesha msimulizi kuwa na uwezo wa kumaizi na kuelewa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, hadithi na mwelekeo wa saikolojia ya viumbe wa hadithini (Wamitila, 2006). Aina hii ya uolezi imetumika katika riwaya ya Kiswahili. Kwa mfano, katika *Harufu ya Mapera*, uolezi nje unadhihirika wakati msimulizi-muolaji anaposema:

Marafiki zake walimshauri awaajiri walinzi lakini hakutaka. Alihisi kwa kufanya hivyo atakosa uhuru wake. Isabelle ambaye zamani alikuwa na walinzi wake kabla ya kumwambia baba yake hataki walinzi alimweleza hayo. Alihisi kama anakabwa koo ya maisha yake, kila anakoenda anafuatwa. La. Alitaka uhuru wa kufanya alivyotaka bila kuwa na hofu ya kuchunguzwachunguzwa kwenye matendo yake (uk. 329).

Msimulizi ambaye ni muolaji nje anasimulia matukio yanayomhusu Isabelle. Mhusika Isabelle ndiye muolaji ndani lakini msimulizi yuko mahali fiche akimfuata mhusika huku akiyasimulia yale yanayomhusu katika maisha yake. Kupitia uolezi nje tunaweza kuuona mtazamo wa Isabelle, mapendeleo yake, taaluma na hata tabia zake. Msimulizi-muolaji anawafahamisha wasomaji kuwa Isabelle alikuwa mwanamitindo na mwanawe mwanasiasa mashuhuri ambaye alikuwa ameshinda mataji mbalimbali ya urembo. Kwa kuwa alikuwa anajiweza kiuchumi, basi, alitaka kuishi maisha yake bila kufuatiliwa na walinzi wa baba yake, kwa sababu, alipenda kustarehe na vijana wenzake bila kizuizi. Kwa hivyo, aliamua kuhama kwao na kuishi peke yake katika mtaa mmojawapo jijini. Uamuzi huu unamfanya kujihusisha kimapenzi na mwana wa mpinzani wa baba yake kisiasa bila ufahamu wa yeyote aliyehusiana na familia yake. Uhuru wa muolaji nje wa kuona na kujua mambo mengi kuhusu hadithi unatuwezesha kufahamu siri za Isabelle. Aidha, uamuzi wake wa kudai uhuru wake unaonesha itikadi ya vijana hasa wale ambao wanatoka katika tabaka la juu hasusani tabaka la wanasiasa ambao huwa wamezuiliwa kutangamana na wenzao kutokana na uadui wa kisiasa kati ya wazazi

wao. Isabelle anakuwa mmoja wa wanamapinduzi ambao wanataka kuondoa chuki za kisiasa miongoni mwa jamii za nchi yake. Hatimaye anaamua kuolewa na Jimna kisirisiri na kutoroka nchini kwa muda.

Kule kutohusika kwa msimulizi katika matukio ya hadithi pia kunamsaidia msimulizi-muolaji kutoathirika na hisia za mhusika, jambo linalomfanya kusimulia na kuyatazama matukio vyema. Hata hivyo, wakati hisia za wahusika zinaposimuliwa, msomaji anaweza tu kupokea yale ambayo msimulizi ameweza kumsimulia wala si kama ilivyo katika uolezi ndani ambapo hisia huwa ni za mhusika mwenyewe. Hisia za Hamza katika *Haini* zinabainika kutokana na uolezi nje kama ilivyo katika muktadha huu:

Hamza, yeye alipwaya pale alipokaa. Amekwisha, kifefe, shahamu yote aliyokuwa nayo imeyeyuka kwa njaa ya gerezani. Nyama iliyokuwa ndani ya kisahani chake ameimaliza, anatamani kuomba “serwa” lakini atathubutu wapi kufanya hivyo. Pale alipo yeye ni kama paa miongoni mwa simba, wanamsubiri afurukute tu wamrarue vipande vipande. Hofu na wasiwasi tele moyoni. Hajui lilompeleka pale... (uk. 80).

Maelezo haya yanaonesha kuwa uolezi unafanyika kipanorama kutokana na kutumia upeo wa jicho la ndege; yaani, muolaji anakuwa sehemu iliyo juu ya kiolwa. Wasomaji wanaweza kumwona Hamza katika hali ya udhaifu kupitia msimulizi-muolaji ambaye ndiye anamwona kwa niaba ya wasomaji. Anasema kuwa Hamza alikuwa na wasiwasi, lakini msomaji hajui kiasi gani cha wasiwasi alichokuwa nacho na jinsi alivyokuwa akihisi alipojipata yuko katikati ya maafisa katili ambao walijulikana kutokana na uhayawani wao. Hatufahamu pia iwapo kweli Hamza alitaka kuomba kitoweo kingine cha nyama ama alikuwa ametosheka na kile cha kwanza ila tunamwamini tu msimulizi-mfokasi ambaye anatuelezea hayo.

Kama tulivyosema hapo awali, uolezi nje pia humruhusu muolaji kuwa mahali anakoweza kuyafuatilia matukio mbalimbali kwa wakati mmoja (Bal, 1985). Kwa mfano, katika *Haini* muolaji anaweza kuyaona yale yanayotendeka ndani, nje na hata juu kwenye mnara kama ifuatavyo:

Koplo Ngwali alikuwa amesimama makini juu ya mnara wa ulinzi. Bunduki iko begani anaangaza kila pembe ya gereza. Mnara wa ulinzi umeinuka juu ukalipita kuta lililozunguka gereza. Palikuwa na minara sita kama ule, mmoja katika kila pembe ya gereza na pale alipo Koplo Ngwali ni katika sehemu ya Kumbakumba, amekwea juu, kila kitu anakiona kimedumaa chini yake. Kaskazini kwake, kilima cha Kinoamiguu kinateremka kwa kasi kuelekea Mivinjeni na kusini kilima hicho kimeinuka ghafula kinapandishia Mazizini. Mashariki ndiko liliko gereza lenyewe,

analitazama kwa pale juu alipo na magharibi majumba ya ghorofa ya Kilimani yamejipanga msururu... (uk. 121).

Katika dondoo hili, uolezi unafanyika kipanorama kutokana na kutumia upeo wa jicho la ndege. Msimulizi-muolaji wa dondoo hili yuko mahali anakoweza kuliona gereza na wakati huohuo kumwona Koplo Ngware mahali alikokaa kwenye mnara. Pia, anaweza kuona jinsi koplo huyo alivyokuwa na uwezo wa kuona kilichokuwa chini yake. Aidha, aliweza hata kufahamu mtazamo wake kuhusu mandhari ya maumbile ambayo hakuwa na haja nayo. Kwa upande mwingine, msimulizi-muolaji huyo aliweza kumwona mfungwa mmoja aliyekuwa ndani ya gereza akijaribu kukwea ngazi ili kuuvuka ukuta uliokuwa umelizingira gereza. Mfungwa huyu hana habari kuwa kule kutikisatikisa waya kulimfanya koplo kufahamu kuwa kulikuwa na jaribio la mfungwa kutoroka. Kwa kuwa msimulizi-muolaji hajulikani mahali maalumu aliko, inakuwa rahisi kwake kufuatilia matukio yanayoendelea na kusimulia kila hatua bila ya kuathirika na matendo hayo. Mfano ufuatao unadhihirisha uolezi unaofanyika kipanorama:

Alimfyatulia risasi ikapita “zuum!” juu ya kichwa chake. Sururu akajiachia, akaanguka chini kwa kishindo kikubwa. Ameshafika nje ya gereza. Damu zimachirizika, mguu umeteguka, mauti yanamkabili, Koplo Ngwali anazifyatua risasi kama mwendawazimu. Sururu alipotelea vichakani kama paa, hakujali damu wala mguu kuteguka, mpango wa Kata Mbuga umeanza (uk. 122).

Katika mfano huu, msimulizi-muolaji anaelezea jinsi ambavyo Koplo alimfyatulia risasi huku risasi hiyo ikipita juu ya kichwa chake. Aidha, anasimulia jinsi mfungwa alivyoraruliwa na waya tumboni kisha kutokwa na damu tumboni mwake, mikononi na hata miguuni. Huenda Sururu hakufahamu hatari iliyomkabili alipojaribu kuvuka ukuta wa gereza, lakini muolaji nje anaweza kuona hatari iliyomkabili wakati risasi zilipokuwa zikifyatuliwa.

Katika simulizi zilizowasilishwa kutokana na mkabala wa nje, msimulizi-muolaji ana uwezo wa kuyasoma mawazo ya wahusika wake na kusimulia yale yanayoendelea katika akili za wahusika (Jahn, 1999). Kupitia aina hii ya uolezi, wasomaji wanaweza kuyajua yale yanayowapitia wahusika akilini bila ya wao wenyewe kuyasema. Msomaji hufanikiwa kuyafahamu mambo ambayo mhusika hataki yajulikane kwa wenzake. Kwa mfano, katika *Harufu ya Mapera* msimulizi-muolaji anasimulia fikra za wahusika watatu walio katika chumba kimoja lakini kwa kuwa wamekuwa na makabiliano, kila mmoja wao anajaribu kuzuia hisia zake za ndani kama ifuatavyo:

Baba-mtu. Macho pima-ule weupe wa macho umekolea zaidi-pumzi juu juu, akakiumauma kidomo chake, mshipa wa kipajini umetokeza kabisa kama mtu anayewangwa na kichwa, akamgeuzia binti yake mkodoo wa macho uliokuwa na maswali

ya kutaka kujua huyu mwanamume amepata ujasiri wa kusema hivi wapi. Wakati huo Isabelle mwenyewe alikuwa anamfanyia ishara za macho Caliban aache mzaha wake. Unatishia kutumbuka usaha huu. Ndiyo anaupenda utani wake tangu zamani lakini anaona huu wa sasa unachukua mkondo usiopendeza (uk. 430).

Kupitia usimulizi maizi ambao unaibua uolezi nje, msimulizi ameweza kusimulia kisa kinachowahusu wahusika watatu. Ngazi ya saikolojia inajitokeza wakati ambapo msimulizi anayasimulia yale yanayojitokeza katika akili ya wahusika hawa. Baada ya Caliban kumwambia Pipo (baba yake Isabelle) kuwa hata yeye anaweza kuwa mume wa mwana wa nyumba kuu, Pipo hafurahishwi na kauli hiyo kwa kuwa kulingana naye Caliban alitoka katika tabaka la chini, hivyo basi, hapakuwa na uwezekano wa yeye kuhusiana na mwanawe ambaye alitoka katika tabaka la juu. Msimulizi-muolaji ameweza kutuonesha fikra za watatu hawa katika muktadha huu mmoja. Caliban angefurahi sana iwapo angeruhusiwa kuoa mwanamke wa tabaka la juu. Kwa upande mwingine, Isabelle alichukulia kila kitu alichokisema Caliban kuwa mzaha, naye Pipo hakuona uwezekano wa jambo kama hilo kutendeka hasa kwa bintiye. Mawazo ya watatu hawa yanatangaza itikadi kuhusu utabaka ulioko katika jamii husika na jinsi kila tabaka linavyojaribu kuidhibiti au kuiondoa mipaka hiyo. Wale wa tabaka la chini wanajaribu kuvuka mipaka ili kulifikia tabaka la juu kupitia njia mbalimbali kama vile ndoa, ilhali walio katika tabaka la juu hawataki kuwa na uhusiano wa kindoa na wale walio katika tabaka la chini. Jambo hili linazua mgogoro katika kijamii.

Aidha, uolezi nje unamwezesha msomaji kuyajua yale mambo ambayo wahusika wengine wanawapangia wahusika wenzao bila ufahamu wao. Hili linadhihirika katika *Ndoto ya Almasi* ambapo msimulizi-muolaji anaweza kuona mipango ya watu wa jamaa ya Masasi wanapopanga mazishi yake bila ufahamu wake. Muolaji anawaona katika shughuli hiyo kama anavyosimulia:

... Watu waliketi kitako wakasifu na kukashifu na kuhesabu mali na watoto wa 'Marehemu'... Akina mama kadha tofauti tofauti waliinuka kwenye hafla na kudai walikuwa wamezaa watoto na 'Marehemu'... Walikuwa jumla ya watoto kumi na sita. Mmojawapo wa watoto hao alikuwa mzee mmoja mwenye madevu na mashurubu ukimtaazama vizuri utasema labda ni nduguye mzee Masasi... (uk. 71).

Masasi hana ufahamu wa yote yanayotendeka nyumbani kwake alipokuwa amefungiwa kule Kisumu baada ya rabsha kutokea kufuatia kifo cha mwanasiasa Tom Mboya. Baada ya rabsha hizo, tetesi zilikuwa zimeenea nyumbani kwao kuwa alikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wameuawa wakati askari walikuwa wanakabiliana na wananchi. Rafiki yake wa karibu, Fwamba, ndiye aliyekuwa amezileta habari za kifo chake. Kwa hivyo, kama desturi, mazishi yake yalipangwa.

Katika kipindi cha maombolezo, mambo mengi yalijitokeza yaliyowaacha wengi vinywa wazi. Kwa mfano, akina mama kadhaa wanajitokeza na watoto kumi na sita wakidai kuwa watoto hao wote walikuwa wa Mzee Masasi. Kwa kuwa mzee huyu hakuwapo, watu walidhani kuwa wangepanikiwa kukirithi kishamba chake. Hali inabadilika ghafla wakati mzee huyo anatokea bila ya waombolezaji kutarajia. Kupitia uolezi nje msimulizi anaelezea hali hiyo:

... ndipo kwa ghafla Mzee Masasi alipotokea, anatembea kwa mwendo wake wa kuyonga. Sokomoko lililofuatia halikutarajiwa. Watu walinyanyuka na kuomba miguu iwaponye nakama. Akina mama wenye watoto wa sura ya Masasi na watoto wenyewe walitoweka, hata Fwamba. Hakuna aliyewahi kuwasikia tena (uk. 72).

Mipango yote ya mazishi na urithi wake ilikuwa inaendelea pasi na Mzee kufahamu. Lakini kupitia muolaji nje aliye mahali fulani akiyashuhudia haya, anaweza kusimulia jinsi kila kitu kilivyotukia hadi wakati ambapo Masasi aliwasili nyumbani kisha wale waliokuwa wanataka kunufaika kutokana na kifo chake wakatoweka.

Kimasafa, viwakilishi kama vile huko na kule vinatumiwa ili kuonesha mahali aliko msimulizi-muolaji (Simpson, 1993). Viashiria hivi pia vinaonesha kujitenga kwa msimulizi kutokana na matendo, hasa maovu. Umbali uliopo unaweza kudhihirisha msimamo wa msimulizi-muolaji kuhusu matukio yanayoendelea. Kwa mfano, katika *Haini*, msimulizi anatumia viwakilishi vya umbali ili kuonesha ukatili uliokuwa ukitendeka katika jela kama ifuatavyo:

Huko ni jela ndani ya jela, wanakosokomezwa wale manunda wasiosarifika. Ndio maana wanakuita chumba cha kiza. Huko ni maskani ya watoto wanaotoroka walinzi wakijaribu kujitangazia uhuru. Huko ni maskani ya wababe wanaothubutu kuvunja amri za gerezani na kukabiliana na askari wakatiana nao masumbwi. Huko huingizwa machepe na madamsi wa gerezani wanaowabughudhi na kuwaonea wafungwa wenzao. Huko ndiko chumba cha kiza (uk. 85).

Dondoo linadhihirisha umbali wa msimulizi-muolaji kutokana na vitendo vinavyoendelezwa katika chumba kimoja cha kiza katika jela la Kumbakumba. Kiashiria hicho kimejitokeza mara kadhaa katika muktadha huu ili kuonesha jinsi ambavyo msimulizi hangependa kukaribia chumba hicho kutokana na madhila yaliyokuwa yakiendelezwa huko. Wafungwa waliofikishwa huko walikuwa wale ambao walionekana kutokubaliana na masharti ya askari gereza kama vile kulazimishwa kukubali makosa yasiyo yao. Katika chumba hiki, mfungwa hakuruhusiwa kuvaa nguo wala kupewa chakula. Aidha, alikabiliana na joto kali lililotoka jikoni na kuumwa na mbu walioonekana kana kwamba walitumwa

kummaliza. Wafungwa wengi waliowahi kufikishwa hapo walikuwa na kumbukumbu za kutisha na hakuna hata mmojawao aliyetamani kurudi huko tena.

Waandishi wa riwaya za Kiswahili wametumia majarida, makala na vitabu mbalimbali katika riwaya zao, huku wengine wakitumia vyombo vya habari kama njia ya kuwasilisha ujumbe. Usomaji wa vitabu, majarida na makala hayo au upashwaji wa habari kupitia vyombo vya habari katika riwaya husika unadhihirisha uolezi nje kwa msomaji au msikilizaji. Katika *Makuadi wa Soko Huria*, mhusika-muolaji anabadilisha uolezi wake kutoka kwa uolezi ndani hadi kwa uolezi nje anapoyasoma yaliyokuwa yameandikwa kwenye makala ya jarida moja kama ilivyo katika mfano ufuatao:

Kusudi la mpango huu lilikuwa ni kuwawezesha wananchi wa maeneo haya wayatumie mazingira yao, wafaidike, na wakati huo huo wasiyaharibu. Mpango huo ulikuwa umekwisha tayarishwa kutoka mwanzoni mwa miaka ya sitini, nao ulitenga sehemu maalumu kwa ajili ya kilimo... (uk. 61).

Kupitia makabrasha hayo, Msakapanofu anapata habari kamili kuhusu jinsi eneo la Delta lilivyokuwa na mradi wa utunzaji mazingira ambao ulikuwa umefadhiliwa na wafadhili kutoka Norway. Mpango wa mradi huo ulikuwa umekamilika na wananchi tayari walikuwa wameelimishwa kuhusu umuhimu wa kupanda mikoko. Baada ya kusoma, Msakapanofu alielewa ni kwa nini eneo hilo bado lilikuwa na msitu mkubwa wa aina hiyo.

Katika *Harufu ya Mapera*, Jude Kinya anasoma kuhusu umuhimu wa mapera kwenye gazeti. Gazeti hilo lilikuwa na makala kuhusu utafiti uliokuwa umefanywa na watafiti mbalimbali ili kutilia mkazo umuhimu wa matunda hayo. Kwa mfano, makala hayo yalisimulia:

Utafiti unaonesha kuwa mapera, ambayo ni matunda yanayokua kwa wingi nchini, na labda ambayo yanadharauliwa na watu wengi ambao wanastahabu kula matunda ya kigeni, yana faida nyingi mwilini. Matunda haya yanathibitishwa na wanasayansi kuwa na kiwango cha chini cha kalori, mafuta na vitamini na madini yana kinga muhimu ya kusafisha mwili... (uk. 501).

Baada ya kusoma makala hayo, Jude anatumaini kuwa mpinzani wake mkubwa wa kisiasa atapata kuyasoma, kwani yeye ndiye aliyekuwa mstari wa mbele kumkejeli kwa kuwa alikuwa akijihusisha na wakulima wa mapera. Aidha, alikuwa na matumaini kuwa nchi yake ingeupa kipaumbele ukulima wa mapera.

Uolezi nje unaweza pia kujitokeza katika simulizi za nafsi ya kwanza hasa wakati ambapo muolaji ndani anasimulia matukio yanayomhusu mhusika au wahusika walio karibu naye (Genette, 1980). Hili hutokea iwapo umbali wa mwanda-wakati na umbali wa kisaikolojia kati ya msimulizi na mhusika ni mfupi. Hali hii ni



muhimu katika uolezi kwa kuwa matumizi ya aina mbalimbali za simulizi humwezesha msomaji kutambua ni nani muolaji wa tukio fulani. Hili linadhihirika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ambayo imesimuliwa kwa kiasi kikubwa katika uolezi ndani. Licha ya kuwa wahusika wakuu wa hadithi hiyo wamepewa jukumu la kusimulia yale wanayoyaona, kwingine, wanatumia uolezi nje ili kusimulia yaliyowahusu wahusika wengine. Kwa mfano, mara kadhaa Nana anachukua jukumu la kusimulia kuhusu Faisal na hata kuwajulisha wasomaji kuhusu mawazo yake kama ilivyo katika dondoo lifuatalo:

Faisal alishangaa. Lakini aliinuka na wote walimpigia makofi. Akenda kuchukua *uud*. Akaketi nao karibu nami. Vipi ataweza kunifuata na yeye hajui nitaimba wimbo gani? Kilikuwa kitendawili changu na chake nadhani. Na yeye pia nadhani alikuwa na wasiwasi. Lakini ile nafsi yangu ya ndani kabisa ilikuja kunisimamia kunambia niimbe tu... (uk. 143).

Licha ya kuwa maneno haya ni ya Nana na yamejitokeza katika nafsi ya kwanza, ukweli ni kwamba, anasimulia kuhusu Faisal ambaye kwa wakati huo alikuwa ameandamana naye ili kwenda katika *Hotel Selwa*. Hili linadhihirika anapotumia neno ‘nadhani’ ili kusimulia hisia za Faisal. Huu ulikuwa wakati ambapo Nana alikuwa amealikwa kwenda katika mashindano ya muziki yaliyokusudiwa kupima uwezo wake wa kuimba. Wakati zamu yake ilipofika, aliamua kuimba bila usaidizi wa ala za muziki zilizokuwapo ila alimwomba Faisal kumchezea ala ya *uud* anapoimba. Kwa kuwa jambo hili halikuwa limepangwa, Nana hakuwa na uhakika iwapo Faisal angeweza kuicheza ala yake kulingana na wimbo wake. Anatumia maneno kama vile “nadhani” kwa kuwa hakuwa na uhakika wa yale ambayo yangetokea baadaye. Naye Faisal hakuwa na habari kuwa jambo kama hilo lingetokea ndiyo sababu anashangaa anapoitwa kucheza *uud*.

#### 4.0 Hitimisho

Mjadala ambao tumeibua katika makala haya umebaini kuwa waandishi wengi wa riwaya za Kiswahili–wana uzoefu wa kutumia uolezi ndani na uolezi nje kama mkakati wa kimsingi wa uwasilishaji simulizi. Hii ina maana kwamba katika michakato mingi ya usimulizi inayojitokeza katika riwaya, kunaibuka mitagusano kati ya uolezi na uhusika ambapo ujumbe mbalimbali uliolengwa kuibushwa na kuwasilishwa kwa hadhira, unawezeshwa kudhihirika. Uhalisia huu umedhihirishwa kupitia uchanganuzi wa riwaya teule zilizotumiwa katika makala haya. Kwa mintarafu ya data iliyotolewa katika riwaya hizi, kunaweza kutolewa mahitimisho ya kijumla kwamba, aina mbili kuu za uolezi zinajitokeza katika viwango na hatua mbalimbali za simulizi husika. Uolezi ndani umefanikishwa kupitia muolaji ambaye yuko ndani ya hadithi ambaye pia anaweza kuwa mhusika katika hadithi hiyo. Uolezi wa aina hii umemwekea msimulizi mipaka ya kusimulia yale anayoyajua. Hivyo basi, matukio ya hadithi huendelea kujulikana kadiri hadithi inavyoendelea kusimuliwa, jambo linalomfanya msomaji kuvutwa karibu na

mhusika-muolaji ambapo hadithi yake inaweza kuaminika kwa haraka. Kwa upande mwingine, hadithi zinazosimuliwa kupitia uolezi nje hazina mipaka ya kisimulizi. Usimulizi wa aina hii humwezesha msimulizi kuwa na uwezo wa kumaizi na kuelewa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, hadithi na mwelekeo wa saikolojia ya viumbe wa hadithini. Aidha, imedhihirika kuwa waandishi wa riwaya za Kiswahili wanatumia mbinu mbalimbali za kisanaa kama vile: hotuba, nyimbo, mashairi na barua miongoni mwa nyinginezo ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe na maudhui ya sampuli mbalimbali ambayo pia huwakuza wahusika.

### Marejeleo

- Abrams, M. H. (1993) *A Glossary of Literary Terms*. New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Bal, M. (1985) *Narratology. Introduction to the Theory of Narrative*. Toronto: University of Toronto Press.
- Barthes, R. (1966) *Introduction to the Structural Analysis of Narratives*. Cambridge: University Press.
- Chachage, S. C. (2002) *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: E&D Limited.
- Chafe, W. (1994) *Discourse, Consciousness, and Time*. Chicago: University of Chicago Press.
- Chatman, S. (1978) *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca: Cornell University Press.
- Clark H. H. na Gerrig R. J. (1990) "Quotations as Demonstrations". Katika *Language*, Juz. Na. 66(4): 764- 805.
- Fowler, R. (1966) *Essays on Style and Language: Linguistic and Critical Approaches to Literary Style*. London: Routledge and Kegan Paul.
- Fowler, R. (1986) *Linguistic Criticism*. Oxford: Oxford University Press.
- Genette, G. (1972) *Narratology*. Inapatikana katika <http://www.signosemio.com/genette/narratology.asp>. Ilisomwa tarehe 1 Julai 2017.
- Genette, G. (1980) *Narrative Discourse: An Essay in Method*. Ithaca: Cornell University Press.
- Gholami, V. (2013) *Conrad and Narrative Theory: A Narratological Reading of Selected Novels of Joseph Conrad*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha London, London.
- Greimas, A. J. (1973) *On Meaning*. Minnesota: University of Minnesota Press.
- Hawthorn, J. (2010) *Studying the Novel: An Introduction* (Toleo la 6). New Delhi: Universal Book Stall.
- Hirsh, J. (2003) *Shakespeare and the History of Soliloquies*. London: Associated University Presses.
- Jahn, M. (1996) "Windows of Focalization: Deconstructing and Reconstructing Concept". *Style*. Juz. 30(2): 241-267. Inapatikana katika [http://www.uni-koeln.de/~ame02/jahn\\_1996.pdf](http://www.uni-koeln.de/~ame02/jahn_1996.pdf). Ilisomwa tarehe 26 Novemba 2018.

- Jahn, M. (2005) *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. English Department: University of Cologne.
- Kagwa, F. M. (2018) *Hujafa Hujaumbika*. Nairobi: Longhorn.
- Leech, G. N. na Short, M. (1981) *Style in Fiction: A Stylistic Introduction to English Fictional Prose*. United Kingdom: Longman.
- Mohamed, S. A. (2010) *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- O'Neil, P. (1994) *Fiction of Discourse: Reading Narrative Theory*. Toronto: University of Toronto Press.
- Prince, G. (1982) *Narratology: The Form and Functions of Narrative*. Berlin: Mouton Publishers.
- Propp, V. (1968) *Morphology of The Folktale*. Austin: University of Texas Press.
- Rimmon-Kenan, S. (2002) *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. (Toleo la 2). London: Routledge.
- Senkoro, F.E.M.K. (1976) *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F.E.M.K. (1987) *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011) *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Shafi, A. S. (2003) *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Short, M. (1991) *Speech Presentation, the Novel and the Press. The Taming of the Text: Explorations in Language, Literature and Culture*. London: Routledge.
- Simpson, P. (1993) *Language, Ideology and Point of View*. United Kingdom: Routledge.
- Tannen, D. (1989) *Talking Voices*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Todorov, T. (1990) *Genres in Discourse*. New York: Cambridge Press.
- Toolan, M. J. (2001) *Narrative: A Critical Linguistic Introduction*. London: Routledge.
- Uspenky, B. (1973) *A Poetics of Composition*. Berkeley and Los Angeles: University of California Press.
- Walibora, K. (2006) *Ndoto ya Almasi*. Nairobi: Moran Publishers.
- Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.
- Wamitila, K. W. (2012) *Harufu ya Mapera*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.